

# Watanzania wahimizwa kulinda amani

NA IRENE MARK

WAKATI Tanzania ikijianda kwa Uchaguzi Mkuu Oktoba 25 mwaka huu, Watanzania wameombwa kuendelea kuilinda amani na utulivu uliopo kwa sababu maisha yataendelea baada ya uchaguzi huo.

Taasisi tatu zilizoandaa mukutano wa kuzungumzia amani na utulivu ni Konrad Adenauer Stiftung (KAS) kutoka Ujeruman, Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD) Baraza la Amani la Viongozi wa Dini Tanzania (IRCPT), mdahalo huo umepewa jina "Maendeleo Dialogue".

Mkutano huo wa siku mbili kuanzia leo utafanyika katika Hoteli ya Serena na mge ni rasmi anatarajiwa kuwa Makamu wa Rais Dk. Gharib Bilal.

Akizungumza ofisini kwake jijini Dar es Salaam jana kwa niaba ya wenzake walioandaa mdahalo huo, Erasto Ndeuka kutoka Taasisi ya KAS, alisema wameamua kuwakutanisha wadau muhimu kwa sababu wanahitaji Tanzania ibakie moja hata baada ya uchaguzi.

Ndeuka alisema mionganoni mwa mambo yanayoweza kulinda amani katika uchaguzi huo ni kuhakikisha unafanyika kwa njia ya haki na amani na ndiyo maana Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Jaji Mstaafu Damian Lubuva amealikwa pia.

Alisema mukutano huo unatokana na makubaliano yaliyofikiwa hivi karibuni na kwamba wadau walikubaliana taasisi hizo zifanye kazi kwa pamoja.